HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA

MTIHANI WA PILI WA KUJISOMEA NYUMBANI KWA DARASA LA SABA 2020

SOMO: MAARIFA YA JAMII

MUDA: SAA 1:30 **JUNI 2020,**

MAELEKEZO

1.Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45)**

2.Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.

3. Andika **jina lako, shule na somo kwa usahihi katika karatasi yako ya kujibia.**

SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA

KIPENGELE CHA I: URAIA

Chagua jibu sahihi kisha siriba herufi ya jibu hilo katika karatasi maalumu ya kujibia uliyopewa

1. Katika alama zifuatazo ni ipi inapatikana katika bendera ya Rais?
   (a) Nyundo (b) Pembe za ndovu (c)Nembo ya Taifa (d) Ramani ya Tanzania (e) Ramani ya Afrika. ☐
2. Mtendaji mkuu wa shughuli zote za kila siku katika Halmashauri ya Manispaa ni_____ (a)Mwenyekiti wa Halmashauri ya Manispaa (b) Mheshimiwa Diwani (c) Meya wa Manispaa (d) Mkurugenzi mtendaji wa Wilaya (e) Mkurugenzi mtendaji wa Manispaa. ☐
3. Maana ya chama kushika hatamu ni _____(a) Chama cha kutoa sera za nchi (b) Chama kuwa madarakani na kuongoza nchi (c) Ni chama kupata nafasi ya kuunda serikali (d) Chama kuwa na viti vingi Bungeni. ☐
4. Bendera ya Taifa la Tanzania unaweza ukaiona katika nchi nyingine na kwenye sehemu ipi? (a) Wanakoishi watanzania (b) Kwenye mji mkuu wa Nchi (c) Anakoishi au ofisi gani anayotembelea mwakilishi wa Tanzania (d) Nchi marafiki ☐
5. Spika wa Bunge la Jamhuri hupatikanaje? (a) Kuteuliwa na Rais (b) Kuteuliwa na Baraza la Mawaziri (c) Huchaguliwa kutoka chama cha wabunge wengi (d) Huchaguliwa na wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano (e) Huteuliwa na msajili wa chama. ☐
6. Ili mtu aweze kupiga kura katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ni lazima awe na sifa zote zifuatazo **isipokuwa** ____ (a)Awe mkazi wa Tanzania (b)Awe ni mtu mwenye umri zaidi ya miaka 18 (c)Awe ni mwenye akili timamu (d) Awe raia wa Tanzania (e) Awe amejiandikisha kupiga kura. ☐
7. Moja kati ya sababu zifuatazo ilichangia kuvunjika kwa Jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki mwaka 1977.

(a) Vita vya Kagera vya mwaka 1978 (b) Tofauti za lugha miongoni mwa nchi wanachama (c) Tofauti kubwa ya kimaendeleo kati ya nchi wanachama (d) Kukosekana kwa makao makuu ya umoja huo (e) Tofauti ya Elimu miongoni mwa viongozi. ☐

8. Ni nani kati ya viongozi wafuatao anakuwa Mbunge moja kwa moja kutokana na wadhifa alionao? ___ (a) Mwanasheria Mkuu wa Serikari (b) Mkuu wa Mkoa (c) Waziri Mkuu (d) Naibu Spika (e) Jaji Mkuu. ☐
9. Katika Nembo ya Taifa pembe za ndovu zinamaanisha nini?
   (a) Umoja (b) Mazao ya biashara (c) Uhuru (d) Mali asili (e) Madini ☐
10. Chombo kinachohusika katika kuandaa na kuendesha chaguzi mbalimbali za viongozi nchini Tanzania ni _____ (a) Bunge (b) Tume ya Taifa ya Uchaguzi (c) Kamati ya uchaguzi ya Zanzibar (d) Mahakama kuu (e) Kamati ya uchaguzi ya visiwani. ☐
11. Dunia huchukua muda gani kujizungusha nyuzi 75 katika mhimili wake?_____
    (a) Saa 5 (b) Saa 24 (c) Saa 3 (d) Saa 1¼ (e) Saa 75 ☐
12. Vyombo vipi kati ya hivi vinahusika na haki za wanawake? (a) UWT na UMATI (b) TAMWA na TAWLA (c) TNGP na BUNGE (d)Mahakama ya UWT (e) BAKITA ☐

KIPENGELE CHA II: HISTORIA

13. Ugunduzi wa moto ulifanyika katika Zama zipi za mawe_____.
    (a) Zama za Kale (b) Zama za kati (c) Zama za mwisho (d) Zama za chuma (e) Zama za kale na kati. ☐
14. Nchi ya kwanza kupata Uhuru Afrika Mashariki ni _____
    (a) Zanzibar (b) Tanzania (c) Kenya (d) Uganda (e) Uganda na Tanzania ☐
15. Wafanyabiashara wa mwanzo kutoka nje ya Afrika kufika Tanzania walitoka bara la ____ (a) Afrika (b) Amerika (c) Asia (d) Ulaya (e) Australia ☐
16. Mfanyabiashara maarufu Tippu Tip alijulikana pia kwa jina la _____ (a) Rashid bin Mohamed (b) Seyyid Said (c) Hemed bin Mohamed (d) Musa Nzuri (e) Majid bin Said ☐
17. Mkutano wa Berlin ulifanyika mwaka 1884 hadi 1885 ulilenga _____ (a) Kukomesha biashara ya Utumwa (b) Kuanzisha mfumo wa vyama vingi katika Makoloni (c) Kugawana maliasili za Ulaya (d) Kutangaza Utalii wa Afrika (e) Kuligawa bara la Afrika mikononi wa wakoloni ☐
18. Biashara ya Utumwa katika Afrika ya Mashariki ilikomeshwa kabisa mwaka _____ (a) 1822 (b) 1845 (c) 1859 (d) 1873 (e) 1880 ☐

19. Waziri mkuu wa kwanza baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961 kutoka kwa Uingereza _____ (a) Rashidi Kawawa (b) Moringe Edward Sokoine (c) Cleopa Msuya (d) J.K. Nyerere ☐
20. Aina ya unyonyaji ambao hujitokeza kwa nchi iliyopata uhuru lakini inatawaliwa kisiasa, kiutamaduni ni _____ (a) Ubepari (b) Ubeberu (c) Ukoloni Mamboleo (d) Ukoloni Mkongwe (e) Ukabaila ☐
21. Familia pana inafananishwa zaidi na kikundi jamii kiitwacho _____
(a) Kabila (b) Jamii (c) Nasaba (d) Jirani (e) Kijiji ☐
22. Jumla ya taratibu zinazohusu maisha ya kila siku ya binadamu huitwa _____
(a) Historia (b) Utamaduni (c) Desturi (d) Demokrasia (e) Mila ☐
23. Zanzibar ilianza kutawaliwa rasmi na Waingereza mwaka ____
(a) 1913 (b) 1882 (c) 1892 (d) 1885 (e) 1919 ☐
24. Mkutano wa kuligawa bara la Afrika mwaka 1885 uliitishwa katika nchi ya _____
(a) Ufaransa (b) Ujerumani (c) Uingereza (d) Itali (e) Ureno ☐
25. Emil Von Zelewisky aliuawa wakati wa vita vya wajerumani na _____
(a) Wahehe (b) Wanyamwezi (c) Wamatumbi (d) Wandengereko (e) Wasambaa ☐
26. Tanganyika ilipata Rais wa kwanza mwaka _____
(a) 1954 (b) 1961 (c) 1964 (d) 1962 ☐

KIPENGELE CHA II: JIOGRAFIA

27. Jua la utosi huwa kwenye Tropiki Kansa tarehe ngapi?
(a) 21 Machi (b) 22 Desemba (c) 23 Septemba (d) 21 Juni ☐
28. Alama za ramani huonesha _____ (a) Milima na Mabonde (b) Mambo yote muhimu yaliyo katika ramani (c) Mito na makao makuu ya miji (d) Ramani nzima (e) Uoto wa Asili ☐
29. Mbuga za wanyama na makumbusho ya kihistoria ni vivutio kwa _____
(a) Wazungu (b) Watu weupe (c) Wakimbizi (d) Watalii (e) Wenyeji ☐
30. Usafirishaji wa bidhaa au watu kupeleka mahali pengine huitwa _____
(a) Uchukuzi (b) Utalii (c) Biashara (d) Mawasiliano (e) Uhamaji ☐
31. Zao ambalo maua yake ni sumu na hutumika kutengeneza dawa za kuulia wadudu huitwa ___ (a) Kahawa (b) Karafuu (c) Pareto (d) Alizeti (e) Karanga ☐
32. Sehemu za bahari zilizoingia nchi kavu zinaitwa_____ (a) Rasi (b) Mlango bahari (c) Pensula (d) Ghuba ☐
33. Tunaposoma mistari ya gridi tunasoma tarakimu ngapi?
(a) Tatu (b) Nne (c) Sita (d) Ulalo na Wima ☐
34. Yafuatayo ni majanga ya asili ___
(a) Moto na tetemeko la ardhi (b) Mafuriko na Tetemeko la ardhi (c) Mafuriko na vitu (d) Radi na Umeme (e) Ukataji miti na ufugaji ☐

35. Ziwa Victoria huunganisha nchi zipi? (a) Uganda, Sudan na Somalia (b) Uganda, Tanzania na Kenya (c) Kenya, Ethiopia na Angola (d) Rwanda, Burundi na Malawi (e) Msumbiji, Zambia na Zimbabwe ☐
36. Kama Marekani iliyoko nyuzi 60^0 Magharibi ni saa 2:00 ni muda gani karika visiwa vya Comoro vilivyoko nyuzi 45^0 Mashariki? (a) Saa 9:30 Alasiri (b) Saa 3:30 Asubuhi (c) Saa 6:30 Mchana (d) Saa 9:00 Alasiri (e) Saa 2:30 Asubuhi ☐
37. Mimea yenye miiba na mizizi mirefu hupatikana katika sehemu zipi? _____ (a) Kiikweta (b) Kijangwa (c) Kimediterrania (d) Kitropiki (e) Vuguvugu ☐
38. Mji wa Accra-Ghana na London Uingereza umepitiwa na mstari upi wa kubuni katika ramani? (a) Longitudo (b) Ikweta (c) Greenwich (d) Tropiki ya Kansa (e) Tropiki ya Kaprikoni ☐
39. Ni kipimo kipi cha ramani kinafaa kwa kuchora ramani ya shule? _____ (a) Kipimo cha kati (b) Kipimo kidogo (c) Kipimo kikubwa (d) Kipimo cha mstari (e) Kipimo cha sehemu. ☐
40. Binadamu wa Kale alianza kula chakula kilichochomwa au kupikwa katika Zama zipi za mawe?
(a) kati (b) mwanzo (c) mwisho (d) mwanzo na kati (e) kati na mwisho ☐

SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Jibu maswali yafuatayo kwa kujaza kwenye nafasi zilizo wazi katika karatasi ya kujibia uliyopewa

41. Chama kipi cha Siasa kiliundwa baada ya kuungana kwa ASP na TANU? _____.
42. Taja madhara mawili ya vita vya Majimaji.
a)_____ b) _____.

SOMA RAMANI YA KONTUA KWA MAKINI KISHA JIBU MASWALI YAFUATAYO:-



43. Taja tofauti kati ya Kontua moja na nyingine katika ramani. _____
44. Mstari wa Kontua uliooneshwa na herufi D ni mita ngapi? _____.
45. Mstari wa Kontua uliooneshwa na herufi G ni mita ngapi? _____.